

A Ni nani aliye huru? Warumi 8:1.

- ❖ Ni wale tu walionauhusiano imara na Kristo wanaweza kuwa huru; hiyo hujumuisha muungano uliochangamka wa kila siku pamoja Naye.

B Tunawekwa huru dhidi ya nini? Warumi 8:2.

- ❖ Tofauti na sheria ya dhambi, sheria ya Roho huleta uhuru na uzima. Sheria ya dhambi huleta mauti na hukumu ya milele pekee.

C Tunawezaje kuupata Uhuru? Warumi 8:3.

- ❖ Sio kwa sheria, kwa sababu ina uwezo wa kutuhumu tu, kwani tu wadhambi.
- ❖ Kupitia maisha na kifo cha Kristo aliyekuwa mwili na kuishi bila dhambi.

D Tuishije baada ya kuwekwa huru? Warumi 8:4.

- ❖ Hatutawaliwi tena na tamaa zetu wenyewe, lakini kwa amri na uongozi wa Roho Mtakatifu anaeishi ndani yetu.
- ❖ Kwa hiyo, kuenenda kwa Roho humaanisha kuishi kulingana na matakwa ya sheria: maisha ya upendo na utii wa upendo.

E Twawezaje kutambua kama tunaishi kulingana na Roho au mwili (Warumi 8:5-8)? Warumi 8:5-8.

❖ KUISHI KULINGANA NA MWILI.

- Kufikiri na kufanya vitu vya mwili.
- Matokeo yake ni dhambi.
- Kukosana na Mungu na kushindwa kumpendeza.
- Kushindwa kuitii sheria ya Mungu.

❖ KUISHI KULINGANA NA ROHO

- Kufanya na kufikiri juu ya vitu vya Roho.
- Matokeo yake ni Amani na uzima.
- Kuwa mwana wa Mungu na kuishi ukimpendeza.
- Hujisalimisha kwa sheria ya Mungu.

F Tunawezaje kuishi tukifikiri mambo ya kiroho? Warumi 8:9-14.

- ❖ Tunakuwa wakiroho pale tunapoongozwa na kuvutwa na Roho Mtakatifu, kwa kumruhusu Yeye kukaa ndani yetu.
- ❖ Roho anaishi ndani yetu panapokuwa na uhusiano wa karibu kati ya Roho na sisi. Hiyo huhusisha kila mara kujisalimisha kwa mapenzi ya Mungu. Roho ana nguvu kubadilisha maisha yetu.

G Je; yapi ni matokeo ya kuishi kwa kufuata Roho? Warumi 8:15-17.

❖ Sasa:

- Tuko huru dhidi ya hofu kwa sababu dhambi zetu zimesamehewa.
- Tunafanywa kama watoto wa Mungu.
- Mungu ni baba yetu na anatutunza.
- Ni warithi wa Mungu kwa sababu sisi ni watoto wake.
- Yesu hushiriki urithi wake pamoja nasi.
- Tunateseka pamoja na Kristo.

❖ Baadaye:

- Tutarithi ufalme wa utukufu na uzima wa milele.
- Tutatukuzwa pamoja na Kristo.